ULEVI

Nipashe Alhamisi Juni 4, 2026 Pg 9.

# Dereva basi la shule anaswa na kilevi akiwa amebeba wanafunzi

**Na Mary Mosha,** *MOSHI*
0715086344 WhatsApp / SMS

HALI ya usalama wa wanafunzi wanaotumia usafiri wa shule mkoani Kilimanjaro imeibua mjadala baada ya dereva wa gari la shule kukamatwa akiendesha akiwa na kiwango kikubwa cha kilevi huku akiwa amebeba wanafunzi 28.

Dereva huyo, Noriega Nathanael, ambaye alikuwa akiendesha gari la shule lenye namba T 288 DWU, alinaswa juzi Juni 2, 2026 na polisi wa usalama barabarani katika operesheni maalumu ya ukaguzi iliyofanyika ndani ya Manispaa ya Moshi.

Kwa mujibu wa polisi, kipimo kilionesha dereva huyo alikuwa na kiwango cha kilevi cha 504, kiwango kinachozidi kwa kiasi kikubwa kiwango kinachoruhusiwa kisheria kwa madereva na ambacho kingeweza kuhatarisha maisha ya wanafunzi aliokuwa akiwabeba pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

Akizungumza baada ya kukamatwa, Nathanael alikiri kutumia pombe kabla ya kuanza majukumu yake ya kila siku, akisema aliamini athari zake zingekuwa zimekwisha kufikia muda wa kuanza safari za wanafunzi.

"Ni kweli nilitumia pombe asubuhi. Nilidhani kufikia jioni ningekuwa sawa, lakini nilipopimwa nilikutwa na kiwango cha kilevi cha 504. Naomba mamlaka zinisamehe au zipunguze adhabu kwa sababu nina watu wengi wanaonitegemea," alisema.

Hata hivyo, kauli hiyo haikuzuia hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yake kutokana na uzito wa kosa hilo.

Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro, ASP Nasoro Sisiwaya, alisema dereva huyo amefungiwa leseni yake ya udereva kwa miezi sita kwa kosa la kuendesha akiwa amelewa.

Alieleza kuwa ulevi ni miongoni mwa makosa makubwa yanayochangia ajali nyingi za barabarani nchini, hivyo polisi hawatosita kuchukua hatua kali dhidi ya madereva watakaobainika kukiuka sheria. "Tunafanya operesheni za kukabiliana na makosa yote hatarishi ikiwemo ulevi, mwendo kasi na upakiaji kupita kiasi. Leo tumemkamata dereva wa gari la shule akiwa na kiwango kikubwa cha kilevi huku amebeba wanafunzi 28. Hili ni kosa kubwa na ni hatari kwa maisha ya watoto," ASP Sisiwaya alisema.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani ya Tanzania, Sura ya 168, Kifungu cha 44 kinakataza mtu kuendesha chombo cha moto akiwa chini ya ushawishi wa pombe au dawa za kulevya kiasi cha kushindwa kukidhibiti ipasavyo.

> **"Hapa tungeweza kupoteza watoto 28 kwa wakati mmoja halafu tukasema ni bahati mbaya. Huu si uzembe mdogo, ni kuhatarisha maisha ya watoto wetu,"**

Vilevile, Kifungu cha 45 kinaharamisha kuendesha gari ukiwa na kiwango cha pombe mwilini kinachozidi kiwango kilichowekwa kisheria, ambacho ni miligramu 80 za pombe katika mililita 100 za damu.

ASP Sisiwaya alizitaka shule zote za msingi, sekondari na vituo vya elimu ya awali kuweka mifumo madhubuti ya kuhakikisha madereva wao wako katika hali salama kabla ya kuanza safari za wanafunzi.

Alipendekeza taasisi hizo kununua vifaa vya kupimia ulevi ili kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara kabla na baada ya safari.

"Tunapomkamata dereva wa shule akiwa amelewa tunalazimika kutafuta usafiri mbadala ili wanafunzi wafike shuleni salama. Hii husababisha usumbufu mkubwa kwa wanafunzi, wazazi na shule husika," alisema.

Katika operesheni hiyo hiyo, polisi pia walimkamata dereva wa bajaji wa eneo la Mbuyuni, Abubakari Ally, kwa kosa la kuwapakia zaidi ya wanafunzi 10 wadogo ndani ya chombo chake.

Kutokana na ukiukwaji huo wa sheria, leseni yake imefungiwa kwa muda wa miezi mitatu.

"Tunawaonya madereva wote wa bajaji kuacha kupakia wanafunzi au abiria kupita kiwango kinachoruhusiwa. Tutachukua hatua kali kwa yeyote atakayebainika kufanya hivyo," ASP Sisiwaya alisisitiza.

Tukio hilo limezua wasiwasi mkubwa miongoni mwa wazazi na wadau wa elimu kuhusu usalama wa watoto wanaotumia usafiri wa shule.

Mkazi wa Moshi, Letisia Temba, alisema hatua ya dereva kuendesha akiwa amelewa ilikuwa sawa na kucheza kamari na maisha ya watoto.

"Hapa tungeweza kupoteza watoto 28 kwa wakati mmoja halafu tukasema ni bahati mbaya. Huu si uzembe mdogo, ni kuhatarisha maisha ya watoto wetu," alisema.

Kwa upande wake Ngasa Silayo alisisitiza umuhimu wa shule kuanzisha kamati maalumu za usalama wa wanafunzi ili kufuatilia hali ya magari na mwenendo wa madereva.

Naye Hasani Juma wa Pasua alisema wazazi wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kufuatilia mazingira ya usafirishaji watoto wao badala ya kuishia kulipa ada za usafiri pekee.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kupitia Ibara ya 14 inatambua haki ya kila mtu kuishi na kupata ulinzi wa maisha yake kutoka kwa jamii na dola.

Wataalamu wa sheria wanaeleza kuwa usafirishaji wanafunzi katika mazingira yasiyo salama unaweza kuhatarisha utekelezaji haki hiyo ya msingi.

Vilevile, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inasisitiza wajibu wa wadau wote kuhakikisha watoto wanapata mazingira salama ya kujifunzia, huku Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiendelea kuhimiza usalama wa wanafunzi kuanzia nyumbani, shuleni na katika mifumo ya usafiri wanaotumia kila siku. Msaikolojia Tiba Edward Mwendamseki alisema watoto wanaowekwa katika mazingira yenye msongamano mkubwa au yanayowatia hofu wakati wa safari wanaweza kuathirika kisaikolojia.

CamScanner